

KUMB: PPR/15 - 12/1

**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU BEI KIKOMO ZA MAFUTA AINA YA PETROLI KUANZIA
JUMATANO, TAREHE 2 Desemba 2015**

Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) inatangaza bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli hapa nchini. Bei hizi zitaanza kutumika kuanzia **Jumatano, Tarehe 2 Desemba 2015**. Pamoja na kutambua bei kikomo za bidhaa mbalimbali za petroli nchi nzima, ni muhimu kuzingatia yafuatayo:-

- (a) Bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa zimebadilika ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 4 Novemba 2015. Kwa Mwezi Desemba 2015, bei za reja reja za mafuta ya Petroli na Dizeli zimeshuka kama ifuatavyo; Sh 28/lita sawa na asilimia 1.38 na Sh 56/lita sawa na asilimia 2.96 sawia, ambapo bei ya Mafuta ya Taa imeongezeka kwa Sh 32/lita sawa na asilimia 1.85, Aidha, kwa kulinganisha na toleo la mwezi uliopita bei za jumla kwa mafuta ya Petroli na Dizeli nazo zimeshuka kama ifuatavyo; Sh 27.64/lita sawa na asilimia 1.45 na Sh 55.68/lita sawa na asilimia 3.14 sawia, na bei ya jumla ya Mafuta ya Taa imeongezeka kwa Sh 31.98/lita sawa na asilimia 1.96. Kwa kiasi kikubwa mabadiliko haya yametokana na mabadiliko ya bei za mafuta katika soko la dunia.
- (b) Kwa mujibu wa Sheria ya Mafuta ya mwaka 2008, bei za bidhaa za mafuta ya petroli zitaendelea kupangwa na soko. EWURA itaendelea kuhamasisha ushindani kwa kutoa taarifa za bei kikomo za bidhaa za mafuta. Taarifa hizi zina lengo la kuwasaidia wadau kufanya maamuzi stahiki kuhusu manunuzi ya bidhaa za mafuta.
- (c) **Kampuni za mafuta zipo huru kuuza bidhaa za mafuta ya petroli kwa bei ya ushindani ilimradi bei hizo ziko chini ya bei kikomo (price cap) kama ilivyokokotolewa na fomula iliyopitishwa na EWURA na ambayo ilichapwa kwenye Gazeti la Serikali Na. 405/2015 la Mwezi Julai 2015.**
- (d) Vituo vyote vya mafuta vinatakiwa kuchapisha bei za bidhaa za mafuta katika mabango yanayoonekana bayana na yakionyesha bei ya mafuta, punguzo, vivutio vya biashara au promosheni zinazotolewa na kituo husika. Pale ambapo inawezekana kuchagua, wateja wanashauriwa kununua bidhaa za mafuta kutoka kwenye vituo vinavyouza mafuta kwa bei ndogo zaidi ili kushamirisha ushindani. **Ni kosa kuuza mafuta bila kuweka mabango ya bei inayoonekana vizuri kwa wateja na adhabu itatolewa kwa kituo husika.**
- (e) Wanunuzi wanashauriwa kuhakikisha kuwa wanapata stakabadhi ya malipo inayoonesha jina la kituo, tarehe, aina ya mafuta yaliyonunuliwa na bei kwa lita. Stakabadhi hiyo ya malipo itatumika kama kidhibiti cha mnunuzi wa mafuta endapo kutajitokeza malalamiko ya ama kuuziwa mafuta kwa bei ya juu kuliko bei kikomo ama endapo utakuwa umeuziwa mafuta yenye kiwango cha ubora kisichofaa.

A: BEI ZA REJAREJA

| Mji | Bei Kikomo | | |
|---------------------------|----------------------|---------------------|----------------------------|
| | Petroli (Sh/Lita) | Dizeli (Sh/lita) | Mafuta Ya Taa (Sh/Lita) |
| Dar es Salaam | 1,977 | 1,823 | 1,765 |
| Arusha | 2,061 | 1,907 | 1,849 |
| Arumeru (Usa West) | 2,061 | 1,907 | 1,849 |
| Karatu | 2,079 | 1,925 | 1,867 |
| Monduli | 2,066 | 1,912 | 1,854 |
| Ngorongoro (Loliondo) | 2,117 | 1,964 | 1,905 |
| Kibaha | 1,981 | 1,828 | 1,769 |
| Bagamoyo | 1,988 | 1,834 | 1,776 |
| Kisarawe | 1,984 | 1,830 | 1,772 |
| Mkuranga | 1,987 | 1,833 | 1,775 |
| Rufiji | 2,004 | 1,851 | 1,792 |
| Dodoma | 2,035 | 1,882 | 1,824 |
| Bahi | 2,043 | 1,889 | 1,831 |
| Chemba | 2,062 | 1,908 | 1,850 |
| Kondoa | 2,068 | 1,914 | 1,856 |
| Kongwa | 2,033 | 1,879 | 1,821 |
| Mpwapwa | 2,037 | 1,883 | 1,825 |
| Iringa | 2,041 | 1,887 | 1,829 |
| Kilolo | 2,045 | 1,891 | 1,833 |
| Mufindi (Mafinga) | 2,051 | 1,897 | 1,839 |
| Njombe | 2,069 | 1,915 | 1,857 |
| Ludewa | 2,107 | 1,953 | 1,895 |
| Makete | 2,100 | 1,946 | 1,888 |
| Wanging'ombe (Igwachanya) | 2,067 | 1,913 | 1,855 |
| Bukoba | 2,192 | 2,038 | 1,980 |
| Biharamulo | 2,166 | 2,012 | 1,954 |
| Karagwe (Kayanga) | 2,208 | 2,054 | 1,996 |
| Kyerwa (Ruberwa) | 2,214 | 2,060 | 2,002 |
| Muleba | 2,192 | 2,038 | 1,980 |
| Ngara | 2,157 | 2,004 | 1,945 |
| Misenyi | 2,200 | 2,046 | 1,988 |
| Geita | 2,142 | 1,988 | 1,930 |
| Bukombe | 2,131 | 1,977 | 1,919 |
| Chato | 2,163 | 2,009 | 1,951 |
| Mbogwe | 2,180 | 2,026 | 1,968 |
| Nyang'hwale | 2,157 | 2,003 | 1,945 |
| Kigoma | 2,208 | 2,054 | 1,996 |

| | | | |
|------------------------|-------|-------|-------|
| Uvinza (Lugufu) | 2,220 | 2,066 | 2,008 |
| Buhigwe | 2,197 | 2,043 | 1,985 |
| Kakonko | 2,165 | 2,011 | 1,953 |
| Kasulu | 2,194 | 2,040 | 1,982 |
| Kibondo | 2,172 | 2,018 | 1,960 |
| Moshi | 2,050 | 1,897 | 1,838 |
| Hai (Bomang'ombe) | 2,054 | 1,900 | 1,842 |
| Mwanga | 2,044 | 1,890 | 1,832 |
| Rombo (Mkuu) | 2,071 | 1,918 | 1,859 |
| Same | 2,037 | 1,883 | 1,825 |
| Siha (Sanya Juu) | 2,057 | 1,903 | 1,845 |
| Lindi | 2,036 | 1,882 | 1,824 |
| Kilwa Masoko | 2,011 | 1,857 | 1,799 |
| Liwale | 2,056 | 1,903 | 1,845 |
| Nachingwea | 2,065 | 1,911 | 1,853 |
| Ruangwa | 2,063 | 1,909 | 1,851 |
| Babati | 2,099 | 1,945 | 1,887 |
| Hanang (Katesh) | 2,109 | 1,956 | 1,898 |
| Kiteto (Kibaya) | 2,110 | 1,956 | 1,898 |
| Mbulu | 2,112 | 1,958 | 1,900 |
| Simanjiro (Orkasumet) | 2,131 | 1,977 | 1,919 |
| Musoma | 2,155 | 2,001 | 1,943 |
| Rorya (Ingirijuu) | 2,164 | 2,010 | 1,952 |
| Bunda | 2,146 | 1,992 | 1,934 |
| Butiama | 2,152 | 1,998 | 1,940 |
| Serengeti (Mugumu) | 2,200 | 2,047 | 1,989 |
| Tarime | 2,166 | 2,012 | 1,954 |
| Mbeya | 2,084 | 1,930 | 1,872 |
| Chunya | 2,093 | 1,939 | 1,881 |
| Ileje | 2,097 | 1,943 | 1,885 |
| Kyela | 2,099 | 1,946 | 1,887 |
| Mbarali (Rujewa) | 2,068 | 1,914 | 1,856 |
| Mbozi (Vwawa) | 2,093 | 1,939 | 1,881 |
| Momba (Chitete) | 2,102 | 1,948 | 1,890 |
| Rungwe (Tukuyu) | 2,093 | 1,939 | 1,881 |
| Morogoro | 2,002 | 1,848 | 1,790 |
| Mikumi | 2,017 | 1,864 | 1,805 |
| Kilombero (Ifakara) | 2,040 | 1,886 | 1,828 |
| Ulanga (Mahenge) | 2,050 | 1,896 | 1,838 |
| Kilosa | 2,020 | 1,866 | 1,808 |
| Gairo | 2,020 | 1,866 | 1,808 |
| Mvomero (Wami Sokoine) | 2,012 | 1,859 | 1,800 |

| | | | |
|-------------------------|-------|-------|-------|
| Turian | 2,027 | 1,873 | 1,815 |
| Mtwara | 2,049 | 1,895 | 1,837 |
| Nanyumbu (Mangaka) | 2,098 | 1,944 | 1,886 |
| Masasi | 2,075 | 1,921 | 1,863 |
| Newala | 2,081 | 1,927 | 1,869 |
| Tandahimba | 2,074 | 1,920 | 1,862 |
| Mwanza | 2,127 | 1,973 | 1,915 |
| Kwimba | 2,163 | 2,009 | 1,951 |
| Magu | 2,135 | 1,981 | 1,923 |
| Misungwi | 2,132 | 1,978 | 1,920 |
| Sengerema | 2,159 | 2,005 | 1,947 |
| Ukerewe | 2,186 | 2,032 | 1,974 |
| Sumbawanga | 2,149 | 1,996 | 1,937 |
| Kalambo (Matai) | 2,142 | 1,988 | 1,930 |
| Nkasi (Namanyeje) | 2,163 | 2,009 | 1,951 |
| Katavi (Mpanda) | 2,184 | 2,031 | 1,972 |
| Mlele (Inyonga) | 2,163 | 2,009 | 1,951 |
| Songea | 2,100 | 1,946 | 1,888 |
| Mbinga | 2,133 | 1,980 | 1,922 |
| Namtumbo | 2,129 | 1,976 | 1,917 |
| Nyasa (Mbamba Bay) | 2,136 | 1,982 | 1,924 |
| Tunduru | 2,159 | 2,005 | 1,947 |
| Shinyanga | 2,105 | 1,952 | 1,893 |
| Kahama | 2,119 | 1,965 | 1,907 |
| Kishapu | 2,134 | 1,980 | 1,922 |
| Simiyu (Bariadi) | 2,147 | 1,993 | 1,935 |
| Busega (Nyashimo) | 2,140 | 1,986 | 1,928 |
| Itilima (Lagangabilili) | 2,150 | 1,996 | 1,938 |
| Maswa | 2,138 | 1,985 | 1,926 |
| Meatu (Mwanhuji) | 2,145 | 1,992 | 1,933 |
| Singida | 2,067 | 1,914 | 1,855 |
| Iramba | 2,079 | 1,926 | 1,867 |
| Manyoni | 2,052 | 1,898 | 1,840 |
| Ikungi | 2,063 | 1,909 | 1,851 |
| Mkalama (Nduguti) | 2,092 | 1,938 | 1,880 |
| Tabora | 2,131 | 1,977 | 1,919 |
| Igunga | 2,085 | 1,931 | 1,873 |
| Kaliua | 2,149 | 1,995 | 1,937 |
| Ulyankulu | 2,143 | 1,989 | 1,931 |
| Nzega | 2,095 | 1,942 | 1,883 |
| Sikonge | 2,142 | 1,989 | 1,931 |
| Urambo | 2,144 | 1,990 | 1,932 |

| | | | |
|------------------|-------|-------|-------|
| Tanga | 1,935 | 1,808 | 1,811 |
| Handeni | 1,955 | 1,829 | 1,790 |
| Kilindi | 1,970 | 1,843 | 1,825 |
| Korogwe | 1,947 | 1,820 | 1,804 |
| Lushoto | 1,956 | 1,829 | 1,814 |
| Mkinga (Maramba) | 1,942 | 1,815 | 1,825 |
| Muheza | 1,940 | 1,813 | 1,811 |
| Pangani | 1,941 | 1,815 | 1,818 |

B: BEI ZA JUMLA

| Bei za Jumla - DSM | Petroli (Sh/L) | Dizeli (Sh/L) | Mafuta ya Taa (Sh/L) |
|---------------------------|-----------------------|----------------------|-----------------------------|
| Bei Kikomo | 1,871.84 | 1,718.12 | 1,659.90 |

| Bei za Jumla - TANGA | Petroli (Sh/L) | Dizeli (Sh/L) |
|-----------------------------|-----------------------|----------------------|
| Bei Kikomo | 1,829.77 | 1,703.00 |

Felix Ngamlagosi
MKURUGENZI MKUU
EWURA